# JARIBIO LA MTIHANI
# DARASA LA SABA - MWAKA 2020
# KISWAHILI:LUGHA

***Muda: Saa 1 Dakika 40***

*SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI*

**1.** Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 50.

**2.** Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-

*(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako*

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne.***

***Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Hati nadhifu ni hati safi. Ni mwandiko ____1____ na matatizo____2____. Herufi ____3____ hutakiwa kuwa sawa. Kuna herufi za kuweka vitone; ni ____4____ vitone hivyo viwepo. Kama ni herufi____5____ kukunjwa chini au juu ya msitari____6____ kukunjwa. Baadhi ya herufi huwa na vistari juu, kwa ____7____, vistari hivyo hupaswa kuwekwa. Mwandiko unatakiwa uwe____8____ wastani____9____ mkubwa sana ____10____ mdogo sana, usomeke vilivyo. Haifai kuka____11____ au kufutafuta kazi iliyoandikwa. Mwandiko____12____ unavutia na ____13____ machoni hata kabla ya mtu kukisoma ____14____ kilicho andikwa. Jifunze kuandika____15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** isiyo | **B.** yasiyo | **C.**usio | **D.**usiwo |
| **2.** | **A.**lolote | **B.**zozote | **C.**yoyote | **D.**yeyote |
| **3.** | **A.**yote | **B.**zote | **C.**wote | **D.**lote |
| **4.** | **A.**nzuri | **B.**vizuri | **C.**uzuri | **D.**zuri |
| **5.** | **A.**za | **B.**la | **C.**ya | **D.**kwa |
| **6.** | **A.**kunafaa | **B.**linafaa | **C.**zinafaa | **D.**tunafaa |
| **7.** | **A.**hilo | **B.**hapo | **C.**zinafaa | **D.**tunafaa |
| **8.** | **A.**kwa | **B.**ya | **C.**wa | **D.**na |
| **9.** | **A.**isiwe | **B.**kusiwe | **C.**zisiwe | **D.**usiwe |
| **10.** | **A.**tena | **B.**pengine | **C.**zaidi | **D.**au |
| **11.** | **A.**katakata | **B.**takata | **C.**kutakasa | **D.**takataka |
| **12.** | **A.**nzuri | **B.**zuri | **C.**mizuri | **D.**mzuri |
| **13.** | **A.**kupendeza | **B.**kupendwa | **C.**kupendesa | **D.**kupendea |
| **14.** | **A.**hiki | **B.**hilo | **C.**kile | **D.**hiyo |
| **15.** | **A.**mzuri | **B.** bora | **C.**viema | **D.**vyema |

***Kuanzia swali la 16-30, jibu swali kulingana na maagizo.***

16. Mahali asimamapo mshukiwa au shahidi mahakamani huitwa
A. mbaroni    B. kizimba
C. dungu    D. vikuku

17. Unda nomino kutokana na sifa **'geni'**
A. ugeni    B. mgeni
C. ugenini    D. geni

18. Badilisha usemi huu kuwa katika usemi halisi
"Leo nitaenda shuleni," Njoroge alisema
A. Nitaenda shuleni kesho, Njoroge alikiri
B. Njoroge alisema kuwa alienda shuleni jana
C. Njoroge alisema kuwa siku hiyo angeenda shuleni
D. Shuleni nilienda siku iliyopita Njoroge alisema

19. Akisami hii $^{1}/_{9}$ ni:
A. Ushuri    B. Sudusi
C. Thumni    D. Tusui

20. Neno **marashi** liko katika ngeli gani?
A. LI - YA    B. YA - YA
C. I - ZI    D. A - WA

21. Kati ya wadudu hawa yupi si kimelea
A. mchwa    B. kunguni
C. kifunza    D. utitiri

22. Kikembe cha mbuzi huitwa
A. kibebe    B. kinengwe
C. kimeme    D. kidue

23. Mtu mwenye elimu ya nyota ni
A. sogora    B. mhasibu
C. mhariri    D. mnajimu

24. Tambua umbo hili



A. kipenyo    B. mche
C. tao    D. kopa

25. Ni ipi si kisawe cha pesa
A. fulusi    B. ngwenje
C. darahima    D. jabali

26. **Andika kinyume cha sentensi**
***Mengi safi yalianikwa uani***
A. Machache machafu yalianuliwa nyuani
B. Mengi machafu hayakuanikwa uani
C. Mengi machafu yalianikwa uani
D. Machache machafu yalianuliwa uani

27. Nahau 'kufuata njia ya marahaba' ina maana ya
A. kutumia njia nzuri
B. kuaga dunia
C. kukimbia mbio
D. kuzingatia sheria

28. Tunasema mfupi kama nyundo ilhali tunasema chungu kama
A. shubiri    B. pilipili
C. halua    D. asali

29. ______huvaliwa masikioni na_____kifuani.
A. kipuli, furungu    B. ndonya, toja
C. kipuli, kidani    D. kishaufu, kipini

30. **Wingi wa sentensi hii ni**
***Wadhifa ule ulimfaa sana binti huyo***
A. Nyadhifa zile ziliwafaa sana mabinti wale
B. Wadhifa zile ziliwafaa sana binti hao
C. Wadhifa zile ziliwafaa sana mabinti wao
D. Nyadhifa zile ziliwafaa sana mabinti hao

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Mwangi aliishi maisha ya ukiwa katika mtaa hatari kwa usalama wa Tegea. Wakazi wa maeneo yake hawakukosa wala kukoma kumpa kibarua cha kuponoa mikonge na kupalilia mihogo. Mwangi aliishi kwa nguvu za maulana. Hatima yake ilikuwa toka mkononi hadi kinywani, bora mate tumboni. Kazi nayo ilizidi kuwa nyingi kinyume na mapato yake ya shilingi ishirini kwa siku kukimu mahitaji ya jamii yake yenye watoto watano na mama.

Mambo yalimwendea segemnege pale alipopigwa kalamu na mwajiri wake, alipopatikana na jozi za viatu. Maisha yakawa magumu nyumbani. Aila yake ilimtegemea kwa hali na mali, "Mambo yaligonga mwamba."

Mwangi alitamani Izrael amnyakue na kumpeleka kuzimuni. Nyumbani kwake alikuwa nadra kuona moshi ukifuka kwani Mwangi sasa alikuwa maskini hohehahe akiulizwa haungami. Mcha Mungu hakosi, mkono wa Jalali nao haukosei. Maskini yule alipata msamaria mwema aliyemsaidia pamoja na familia yake. Kwa hali na mali. Aliwapa mlo, ajira, elimu na kuwatekelezea maslahi yao yote.

**31.** Kibarua alichopewa Mwangi kilikuwa cha
- A. kuponoa mikonge peke yake
- B. kupalilia mihogo
- C. kuishi kwa ukiwa
- D. kuponoa mikonge na kupalilia mihogo

**32.** Mwangi aliishi maisha ya ukiwa
Haya ni maisha ya
- A. furaha
- B. upweke
- C. upweke na huzuni
- D. upweke na furaha

**33.** Pesa alizozipata Mwangi
- A. zilimsaidia kutenda mambo mengi
- B. ziliishia kwa chakula
- C. zilipotea baada ya kumaliza kazi
- D. zilimsaidia kuishi kwa nguvu za Maulana

**34.** Ni jina gani halimaanishi Maulana?
- A. Mungu
- B. Jalali
- C. Rabuka
- D. Ustadhi

**35.** Mambo kwenda segemnege ni
- A. kuwa shwari kabisa
- B. kuwa na furaha na matatizo
- C. kuwa maskini bila hela
- D. kuharibika na kwenda kinyume na matarajio

**36.** Kwa nini Mwangi alitamani kunyakuliwa na Izraeli?
- A. Alikuwa na furaha
- B. Alitamani kuishi kwa Mungu
- C. Alitaka kupelekwa kuzimuni
- D. Alisongwa na matatizo na dhiki

**37.** Mwishoni Mwangi alisaidiwa na
- A. kasisi
- B. msamaria mwema
- C. Mungu
- D. majirani

**38.** Mwangi alisaidiwa kwa njia zifuatazo ila
- A. kupewa chakula
- B. kuajiriwa kazi
- C. kuelimishwa kwa watoto wake
- D. kupigwa kalamu

**39.** Tunasema ***jozi la viatu***. Pia tunasema jozi la
- A. Nguo
- B. Soksi
- C. Ngozi
- D. Nywele

**40.** Neno nadra linamaanisha
- A. rahisi
- B. kawaida
- C. vigumu
- D. shida

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 41 - 50.***

Ati asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu? Jawabu lake ni vigumu kusema, ndio au la. Bahati ni kwamba Mungu si Athumani na huwabariki wote bila ya kubagua. Hebu jiulize swali hili, mama akifufunza namna ya kuwachomeka wengine mizizi ukubali tu kwa kuwa hutaki kufunzwa na ulimwengu? Je, ni sawa kutaamali msemo ' mtu hakatai wito ila analoitiwa?"

Aghalabu utawasikia wazee wakidai kuwa, mtoto wa nyoka ni nyoka. Naam! Hatupingi wala hatukatai lakini swali ni hili, ni lazima mzazi akiwa pwagu sharti mwana awe pwagu? sidhani ikiwa ni lazima mambo kuwa hivyo na sioni ni kwa nini katika hali hii tumkubalie mwana aliyebebwa kutazama kisogo cha nina.

Fadhili anatoka katika familia adibu. Anapoanza tabia za uchopozi akakanywa na wavyele naye akakataa kenye kenye na mwishowe kulishwa kalenda, inakuwa wazi kuwa asiyesikia la mkuu huvunjika guu, na anapojutia kitendo chake ndipo anapong'amua ya wenye ndimi za kihenga kuwa majuto ni mjukuu.

Mwanfunzi akiwa shuleni hana budi kuwatii walimu wake kwani wao ni mithili ya mfinyanzi alivyo yeye udongo. Anapozuka na mkono mrefu, walimu humwita na kumwonya kwa kumpa nasaha mzomzo. Anapotia komango sikioni na kuyaona yasiyo mhusu ndewe wala sikio na kushikilia kukutu uluja, hubainika wazi kuwa cha kuvunjika hakina fundi.

Kinyume na hayo, mwanafunzi mwenye juhudi humwandama mwalimu kama mtu na kivuli. Kwa kuwa mwalimu ni mjuzi hodari, hubuni mikakati kabambe na kamambe ya kuzinoa akili za mwanafunzi ambaye hufuzu mtihani na kuweka dhahiri shahiri methali kuwa kinolewacho hupata kikakata sawasawa na kuwa mfuatana na mmanga hunukato.

**41.** Mwandishi anapoanza makala, anaonekana kuteswa na uamuzi wa
- A. kama si kweli kuwa asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu
- B. iwapo kuna ukweli katika porojo kuwa asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na dunia
- C. Iwapo kuna siku mtoto asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu
- D. Ikiwa ni kweli kuwa asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu

**42.** Msimamo wa mwandishi ni kuwa Mungu
- A. huwabariki wengine kwa kiasi zaidi
- B. huwanyima wengine baraka akawapa wengine
- C. huwabariki wote bila kubagua
- D. huwafungia wengine milango yote ya heri

**43.** Kifungu "***kuwachomeka wengine mizizi***" hakina maana ya
- A. kuwaloga wengine
- B. kuwafanyia uwanga wengine
- C. kuwafanyia wengine mambo ya usihiri
- D. kuwaangushia wengine kikuti kibichi

**44.** Kwa misingi ya maadili, mwandishi anapinga vikali methali hizi ila
- A. mwana wa nyoka hafunzwi kuuma
- B. bendera hufuata upepo
- C. mwana wa nyoka ni nyoka
- D. mwana wa kuku hafunziw kuchakura

**45.** Kwa kurejelea kifungu, ni dhahiri kuwa mwandishi anaamini sana katika
- A. maadili na utu visizingatiwe mno katika maisha
- B. watu wasifanye wanayoyajua tu
- C. watu wasiwe werevu na kugundua siri katika methali
- D. Maadili na utu vipewe nafasi ya kwanza katika maisha

**46.** Mwandishi anamlinganisha mwalimu na mfinyanzi kwa
- A. Mwalimu huweza kumwongoza mwanafunzi akawa mtu mtajika halafu
- B. Mwalimu huweza kumwongoza mwanafunzi akapita mtihani
- C. Mwalimu anaweza kumzuia mwanafunzi kupata ndoto yake
- D. Mwalimu hana uwezo wa kumfanya mwanafunzi kufuzu katika aushi yake.

**47.** Kifungu ***"anapotia komango sikioni"*** kimetumiwa kifunguni kwa maana ya
- A. Anapotekeleza aliyoambiwa
- B. Anapoyapuuza aliyoambiwa
- C. Anapopokea anayoambiwa
- D. Anaposhughulikia anayoambiwa

**48.** Mwandishi katika hatima ya makala anadhihirisha kuwa
- A. mwanafunzi anayewaandama walimu huonewa na walimu mtihani
- B. mwanafunzi asiyeuliza maswali hawezi katu kufuzu mtihani
- C. mwanafunzi anayewaandama walimu siku zote hufuzu maishani
- D. Mwanafunzi asiyewatii walimu katu hana fanaka katika aushi yake

**49.** Mwandishi amemalizia maandishi yake kwa methali ***'mfuatana na mmanga hanukato'*** ili
- A. kuonyesha ilivyo vigumu kufanya urafiki na watu wenye uwezo
- B. kubanisha hasara za kufanya urafiki na walio na uwezo
- C. kudhihirisha umuhimu wa kufanya urafiki na watu wasio wema
- D. kuonyesha umuhimu wa kufanya urafiki na watu wema

**50.** Ujumbe ambao unajitokeza katika makala haya bila ya shaka ni
- A. Fasili mbalimbali za methali za Kiswahili
- B. Methali za Kiswahili na mitego yake
- C. Matumizi mwafaka ya methali za Kiswahili
- D. Mafumbo yaliyo katika methali za Kiswahili